



طوبہ دگر کے لفظوں میں ایک اہم مانی وصیت (Swahili)

Ubora wa Usamehevu na Uvumilivu

na Wosia Mmoja Muhimu wa Madani



Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal
MUHAMMAD ILYAS
Attar Qadiri Razavi



عفو و درگذر کے فضیلت

‘Afw-o-Dar Guzar ki fazilat

Ubora wa Usamehevu na Uvumilivu na Wosia Mmoja Muhimu wa Madani

Kijitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-Islami ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دامت برکاتہم العالیة
Katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wajulishe Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

Majlis-e-Tarajim (Dawat-e-Islami)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran,
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

UAN: ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 1262

Email: ✉ translation@dawateislami.net

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.
Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَاَنْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf, vol. I, pp. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

Table of Contents

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu	ii
Ubora wa Usamehevu na Uvumilivu	1
Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ	1
Msamaha wa Mtume wa Madanī.....	2
Sababu tatu za hisabu kuwa nyepesi.....	2
Kasri Peponi.....	3
Kusamehe huzidisha utukufu.....	3
Mwenye utukufu zaidi ni nani?.....	4
Asiyesamehe hasamehewi	4
Tabia njema zaidi za duniani na ahera.....	4
Samehe na usamehewe	5
Mtu mwenye kusamehe anaahidiwa msamaha bila hesabu.....	5
Alimsamehe, aliyejaribu kumshambulia.....	5
Dua ya muongozo kwa waliomdhulumu.....	6
Alimsamehe mchawi.....	6
Utukufu wa Mtume mwenye rehema ﷺ	7

Wasamehe mara sabini kila siku	7
Uvumilivu wa ‘Alā-Ḥaḍrat alipopata barua za matukano	8
Wosia muhimu wa Madanī	8
Mifano muhimu kutoka kwa Fatāwā-e-Razawīyah̄.....	11
Aliyebadilisha utambulisho wake!	12
Kusemana vibaya ni Ḥarām	13
Kutimiza masharti yote ya mapatano kwa wale waliotoka kutoka Dawat-e-Islami	14
Ikiwa hutamani kufanya kazi na Dawat-e-Islami kisha.....	15
Ewe Allah عَدَّوَجَلَّ ! Kuwa shahidi wangu.....	17
Vita dhidi ya usengenyaji	17
Nimemsamehe Ilyās Qādirī	19
Ombi la Madanī kwa wanaodai.....	19
Msichana bubu azungunza	20

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Ubora wa Usamehevu na Uvumilivu na Wosia Mmoja Muhimu wa Madani



Shetani atatumia kila hila ili kukuzuia kusoma kitabu hiki, lakini utaingiwa na hofu ya Allah عَزَّوَجَلَّ kubwa baada ya kukisoma
إِنَّ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ.

Ubora wa kumsalia Mtume ﷺ

Maelezo ya rehema kutoka kwa Mfalme wa Makkah na Madinah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ: 'Enyi watu! Hakika, mtu ambaye atapata afueni ya haraka kutokana na hofu na hesabu siku ya Qiyama, ni yule ambaye amenisalia kwa wingi humu duniani.'

(Musnad Firdaus, Juz. 5, uk. 375, Hadithi 8210)

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Msamaha wa Mtume wa Madanī

Ḥaḍrat Sayyidunā Anas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ ameeleza, ‘Siku moja nilikuwa natembea pamoja na Mtume wa rehema صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akiwa amevaa kitambara kizito cha Najrānī¹ chenye pembe zilizo rafu. Ghafla Mbedui mmoja akakishika na kukivuta kwa nguvu ambazo ziliacha alama shingoni mwa Mfalme wa ulimwengu, Kipenzi cha Mola wa ulimwengu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Mbedui halafu akasema, ‘Niombe nipewe sehemu ya mali ambayo Allah عَزَّوَجَلَّ amekupa.’ Rehema ya ulimwengu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alimtazama na akatabasamu na akaamrisha ili apewe sehemu ya mali.’ (Ṣaḥīḥ Bukhārī, Juz. 2, uk. 359, Ḥadīthi 3149)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ndugu waislamu! Je, mumeona namna gani Mtume wetu Kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alivyomshughulikia Mbedui? Enyi wafuasi wa Muṣṭafā! Kwa hali yoyote ile (watu) wakawachokoza au kuwaudhi, muwasamehe na mujaribu kuwachukulia vizuri kwa uvumilivu na mapenzi ya hali ya juu.

Sababu tatu za hisabu kuwa nyepesi

Ḥaḍrat Sayyidunā Abū Ḥurairah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ ameeleza, ‘Mtume Kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Mwenye mambo matatu, Allah عَزَّوَجَلَّ ataifanya hesabu yake kwa wepesi na atamuingiza

¹ Kitambara kipatikanacho sehemu ya Najrān, kusini-magharibi mwa Saudi Arabia.

peponi kwa Rehema yake.’ Maswahaba رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمْ wakauliza, ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ni mambo gani hayo?’ Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akajibu:

1. Mpe anayekunyima.
2. Muunge anayekukata.
3. Msamehe anayekudhulumu.

(Mu’jam Awsaṭ, Juz. 4, uk. 18, Ḥadithi 5064)

Kasri Peponi

Ḥaḍrat Sayyidunā Ubāi Bin Ka’ab رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ ameeleza kwamba Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Anayependelea kujengewa kasri peponi, basi amsamehe yule anayemdhumu na ampe ambaye amemnyima na ajenge uhusiano na yule ambaye anajaribu kuvunja uhusiano na yeye.’

(Al-Mustadrak, juz. 3, uk. 12, Ḥadith 3215)

Kusamehe huzidisha utukufu

Rehema ya ulimwengu, mwisho wa Mitume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Sadaka haipunguzi mali na iwapo mtu atamsamehe aliyemkosea, basi Mola aliyetukuka عَزَّوَجَلَّ humuongozea (aliyesamehe) utukufu na heshima. Anayenyenyekea kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ, Allah عَزَّوَجَلَّ huinua hadhi yake.’

(Ṣaḥīḥ Muslim, uk. 1397, Ḥadithi 2588)

Mwenye utukufu zaidi ni nani?

Ḥaḍrat Sayyidunā Mūsā عَلَى تَيْبَتَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَام amesema, ‘Ewe Allah عَزَّ وَجَلَّ, uliyetukuka! Aliye mtukufu zaidi kwako ni nani?’ Allah عَزَّ وَجَلَّ akajibu, ‘Yule anayesamehe ingawa ana uwezo wa kulipiza kisasi.’ (*Shu’abul Īmān*, juz. 6, uk. 319, Ḥadīthi 8327)

Asiyesamehe hasamehewi

Sahaba Sayyidunā Jarīr رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ ameeleza kwamba Mtume Mtukufu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘asiyehurumia hahurumiwi na asiyesamehe hasamehewi.’

(*Musnad Imām Aḥmad*, juz. 7, uk. 71, Ḥadīthi 19264)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Tabia njema zaidi za duniani na ahera...

Sayyidunā ‘Uqbaḥ Bin ‘Amir رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ amesema kwamba alibahatika kumuona Sultan wa dunia na ahera, Mtume aliyetukuka, Kipenzi cha Allah عَزَّ وَجَلَّ akakurupuka ili aushike mkono uliobarikiwa wa Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Mtume Mtukufu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaushika mkono wake na akasema ‘Uqbaḥ! Tabia njema zaidi za duniani na ahera ni kujihusisha na wale ambao wamejitenga na wewe na uwasemehe wale wanaokufanyia maonevu na anayetaka maisha marefu na ukunjufu katika riziki basi awakirimu jamaa zake.’

(*Al-Mustadrak*, juz. 5, uk. 224, Ḥadīthi 7367)

Samehe na usamehewe

Sultani wa wenye nuru Madīnah-tul-Munawwarah, Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Kuwa na huruma kwa wengine na utamiminiwa huruma na kuwa msamehevu, Allah عَزَّوَجَلَّ atakusamehe.’ (Musnad Imām Ahmad, juz. 2, uk. 682, Hadithi 7062)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Mtu mwenye kusamehe anaahidiwa msamaha bila hesabu

Sayyidunā Anas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ ameeleza kwamba Sultan wa Madīnah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema, ‘Itanadiwa katika Siku ya Hisabu, ‘Wowote wenye zawadi ya rehema ya Allah wasimame na waingie Peponi.’ Kutaulizwa, ‘Ni nani mwenye zawadi hii?’ Anayenadi atajibu, ‘Ni kwa wale wenye kusamehe.’ Kisha maelfu ya watu watasimama na kuingia Peponi bila hisabu.’

(Mu’jam Awsaṭ, juz. 1, uk. 542, Hadithi 1998)

Alimsamehe, aliyejaribu kumshambulia

Katika ukurasa wa 604 wa ‘Sirat-e Muṣṭafā’ [chapisho la kurasa 862 la Maktaba-tul-Madīnah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami], imenukuliwa: Siku moja wakati wa safari, Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa amelala. Wakati huo Ghawraṣ Bin Hārīṣ alitoa upanga wake kwa nia ya kumuua. Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alipoamka, Ghawraṣ akauliza, ‘Ewe

Muḥammad! Ni nani atakayekuokoa kutokana na mimi?’ Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Akajibu, ‘Allah!’ Aliposikia sauti ya utume, alishikwa na woga na (upanga) ukaanguka kutoka mikononi mwake. Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akautwaa upanga na akamuuliza, ‘Sasa, ni nani atakayekuokoa wewe kutoka kwangu?’ Ghawraš akamsihi (Mtume) asimue. Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akamsamehe na akamuachilia aondoke. Ghawraš aliporegea kwa kabila lake, aliwaambia kwamba atoka kwa mtu ambaye ni mbora kulikowatu wote wa ulimwengu.

(Ash-Shifā, juz. 1, uk. 106)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Dua ya muongozo kwa waliomdhulumu

Katika vita vya Uḥud, jino moja la Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, lilivunjika na uso wake ukajeruhiwa lakini Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ hakuwaambia chochote ila: اَللّٰهُمَّ اِهْدِ قَوْمِيْ فَاِنَّهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ (‘Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ waongoze watu wangu, kwa sababu hawanifahamu’).

(Ash-Shifā, juz. 1, uk. 105)

Alimsamehe mchawi

Labīd bin A’ṣam alimrushia uchawi Mtume, lakini Huruma ya Ulimwengu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ hakulipiza kisasi. La ziada, alimsamehe mwanamke myahudi ambaye alimtilia sumu.

(Al Mawāḥib-ul-Ladunniyah lil-Qaṣṭalānī, juz. 2, uk. 91, Dar-rul-Kutub Ilmīyah, Beirut)

Utukufu wa Mtume mwenye rehema ﷺ

Mama wa waumini wote, Sayyīdatunā ‘Āishah Ṣiddīqah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا amesema kwamba Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa hatamki maneno machafu, ya kitabia wala kujikalifisha. Wala hakuwa miongoni mwa wapigaji makelele sokoni, wala hakulipa ubaya kwa ubaya bali alikuwa akisamehe.’

(Jāmi’ Tirmizī, juz. 3, uk. 409, Ḥadīthi 2023)

Wasamehe mara sabini kila siku

Mtu mmoja alikuja katika baraza la Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na akasema, ‘Ewe Mtume! Tuwasamehe wafanyi kazi wetu mara ngapi?’ Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akabakia kimya. Akauliza tena na Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akabakia kimya. Alipoulizwa mara ya tatu, Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akajibu, ‘Mara sabini kwa siku.’

(Jāmi’ Tirmizī, juz. 3, uk. 381, Ḥadīthi 1956)

Mfasiri mashuhuri wa Quran, Mufti Aḥmad Yār Khan Na’imī رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ alishereheshea hadithi hii, ‘Katika lugha ya ki-Arabu mara sabini inarejelea mara nyingi. Kwa hivyo, maelezo yanaashiria kwamba wasamehewe mara kadhaa kila siku. Hata hivyo, tuzingatiye tu kusamehewa katika hali ambayo hawakukusudia au makosa yao yameleta hasara tu kwa mali ya mwajiri wao. Wasisamehewe wanapofanya kosa kusudi kutokana na udhaifu wao au makosa yao yanasababisha hasara kwa watu, au kuvunja sharia ya kidini au nchi.’

(Mirāt-ul Manājīh, juz. 5, uk. 170)

Uvumilivu wa ‘Alā-Ḥaḍrat alipopata barua za matukano

Lau tungekuza hamu ya kutengana na hasira kama vile wacha Mungu waliotutangulia walivyooonesha uvumilivu kwa wengine licha ya udhalimu wao usiokifani. Katika muktadha huu, inaelezwa katika ‘Ḥayāt-e-‘Alā-Ḥaḍrat’ kwamba siku moja barua zilitumwa kwa ‘Alā-Ḥaḍrat, Imām wa Aḥl-us-Sunnāh, Maulānā, Ash-Shaḥ Imām Aḥmad Razā Khān رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ na baadhi yazo zilikuwa zina matusi. Wafuasi wake walighadhabika na wakataka kuwashitaki walioandika barua hizo. Imām wa Aḥl-us-Sunnāh, Maulānā, Ash-Shaḥ Imām Aḥmad Razā Khān عَلَيْهِ الرَّحْمَةُ الرَّحِيمُ akawaambia kwanza wapeni zawadi kwa wale waliowatumia barua za kunisifu halafu ndipo muwashtaki wale waliotuma barua zile za kinitusi. (*Ḥayāt-e-A‘lā Ḥaḍrat, juz. 1, uk. 143*) Yaani ikiwa hamuwapi zawadi wale wanaonisifu basi kwa nini munalipiza kisasi kwa wale wanaonitukana?

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Wosia muhimu wa Madani

Ndugu waislamu! Ninapoandika haya, nakaribia miaka sitini. Kifo kinanikaribia polepole. Nani anayejua ni lini macho yangu yatafumba milele? Ninaomba, kutoka kwa Allah عَزَّوَجَلَّ Mwenye huruma, ulinzi wa imani yangu; amani na utulivu wakati wa kifo changu katika kaburi na Siku ya Kiama. La ziada, ninaomba uokozi bila hesabu Siku ya Kiama na maskani katika

Jannat-ul Firdaus, Pepo ya ngazi ya juu kabisa, jirani na Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Nimeshuhudia mazito kadhaa ya ulimwengu katika maisha yangu mafupi; majivuno mengi na ukosefu wa ukweli; sifa nyingi za uongo na ukosefu wa uaminifu. Hebu fikiria ni usaliti ulioje, ya kwamba mtu anawafukuza wazazi wake mwenyewe kutoka nyumbani kwake kwa sababu ndogo au kwa kutowapenda na akasahau fadhila nyingi na matendo ya huruma mengi kutoka kwao. Lahaula! Shetani aliyelaaniwa, amechafua akili na mioyo ya watu lakini, الْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ mamilioni ya watu wamejiunga na Dawat-e-Islami.

Kama ilivyokawaida ya vyama vikubwa vya kidini, watu huingia na kutoka wanavyopenda, vile vile nimewakuta baadhi ya watu wakikasirika na kujitenga na Dawat-e-Islami. Na baada ya kuwa mbali na mazingira mazuri ya kimadani, baadhi yao wameonekana kuwa na upungufu katika amali zao. Wengine wakaunda makundi yao tofauti. Wengine wamenisema, wameandika mengi kunipinga na wamepinga uamuzi wa Markazi Majlis-e Shūrā ya Dawat-e-Islami.

Licha ya hayo, الْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ, mpaka sasa ninapoandika haya, Dawat-e-Islami inaendelea kufaulu na mpaka sasa hakuna kundi linalokaribia kuwa kiwango sawa na Dawat-e-Islami. Sehemu kubwa ya maisha yangu, nimejishughulisha kujitolea kuihudumia kazi hii hivyo basi kutokana na uzoefu wangu, ninatoa wosia wa Madani kwa ndugu wote waislamu kwa lengo la maisha bora tu ya ahera.

Ninawaomba musingatie kitu kimoja na mushikamane nacho ikiwa niko hai au hata baada ya kifo changu, ukisha jiunga na Dawat-e-Islami, usianzishe kundi lengine lenye mfumo tofauti huku ukawa unaendelea kutumia utambulisho wa Dawat-e-Islami (km. kilemba cha kijani nk.) kwa sababu hata kama utakuwa umeanzisha kundi hilo kwa lengo la kuimarisha kazi za kidini, itakuwa vigumu sana kujiepusha na kusengenywa, kusimanga, dhana, kuvunja moyo wengine, kuwa na uadui kwa waislamu wenzako na chuki. Si wewe tu, bali hata waislamu wengine huenda wakaingia mtegoni katika madhambi haya makubwa.

Ikiwa yeyote anaona kwamba mimi baada ya kujitenganisha na Dawat-e-Islami na kuanzisha kundi lingine nimeweza kufanya kazi kadha wa kadha kubwa kubwa za dini namuomba azingatie kwamba asije akawa amejihusisha na madhambi ya kusengenywa nk. Ikiwa la, basi kongole kwake. Matendo yake mema hayo (ambayo si ya faradhi bali ni ya hiyari) yana uzito zaidi au kusengenywa na dhambi nyingine zina uzito zaidi kesho ahera? Ikiwa moyo wa mtu una hofu ya Allah, na amepata baraka ya elimu ya dini; na ana nuru ya imani basi jibu lake litakuwa hilo tu; kwamba bila shaka uzito wa dhambi moja ya usengenyaji ni nzito zaidi kuliko matendo yake mema yote (ya hiyari) ya maisha. Kwa sababu hakuna adhabu kwa mwenye kuacha tendo jema la hiyari wakati usengenyaji ni dhambi inayoweza kusababisha kupewa adhabu.

Hivyo basi, kuunda kundi lingine baada ya kutoka au kutolewa katika Dawat-e-Islami, مِنْ حَيْثُ التَّجْمُوع (kwa jumla) kunaweza kusababisha hasara.

Mifano muhimu kutoka kwa Fatāwā-e-Razawīyyāh

Kusema kweli ni kwamba utekelezaji kazi yoyote ya kidini isiyokuwa ya faradhi, wajibu au sunna iliyokokotezwa na utekelezaji wake huteteleza chuki miongoni mwa waislamu, basi ni bora kuliambaa hata ikiwa ni jambo linalopendeza kutenda. Ili kudhihirisha umuhimu wa umoja wa waislamu, ‘Alā-Ḥaḍrat, [Imām Aḥmad Razā Khān] رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameeleza: Ili kufurahisha nyoyo za watu na kuunganisha waislamu, inaruhusiwa mtu kuepuka Mustaḥab (jambo linalopendeza kisheria na si la lazima) ili chuki isipate kuingia nyoyo za watu. Kama Mtume mwenye huruma صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alivyodumisha ujengaji wa Ka’bah, kwa mfumo wa Makuraish ili wanaosilimu wasifikwe na dhana mbaya. (*Fatāwā Raḍawīyyāh (Jad id), juz. 7, uk. 680*)

Zaidi ya hayo, imeamrisha kuepuka Mustaḥab (jambo linalopendeza kisheria na si ya ulazima) wakati itazusha chuki miongoni mwa waislamu. ‘Alā-Ḥaḍrat [Imām Aḥmad Razā Khān] رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema kanuni ya ki-Madanī yakuimarisha mapenzi miongoni mwa waislamu: kuchunga nyoyo za watu na mapendekezo yao ni muhimu zaidi kuliko kuchunga utekelezaji wa jambo ambalo limependekezwa na sharia na halina ulazima au kuepuka jambo ambalo limependekezwa

na sharia, halina ulazima au kuepuka jambo ambalo limependekezwa na sharia kuepukwa na halina ulazima. Tusiwe wenye kusababisha fitina, chuki, maudhi na kuwakimbiza watu. [Sheria hii haingii katika kuacha Farḍhi, Wājib na Sunna, iliyokokotezwa. (*Fatāwā Raḍawīyyah (Jad īd)*, juz. 4, uk. 528)

‘Alā-Ḥaḍrat [Imām Aḥmad Razā Khān] رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ amesema sheria moja katika Fiqhi: **مِنْ جَلَبِ الْمَصَالِحِ** yaani ‘Ni muhimu zaidi kuondoa kisababishi cha uovu kuliko kutafuta kisababishi cha wema.’ (*Fatāwā Raḍawīyyah (Jad īd)*, juz. 9, uk. 551)

Aliyebadilisha utambulisho wake!

Wale ambao wamejitenga na utambulisho wa Dawat-e-Islami [kilemba cha kijani nk.] na bila ya misingi ya kisheria za Uislamu, hawaipingi Dawat-e-Islami na wanatoa huduma zao za dini bila kujiingiza katika usengenyaji na uongo; Allah عَزَّوَجَلَّ ayakubali matendo yao mema. Kwa upande mwingine wale ambao wamejitenga na utambulisho wa Dawat-e-Islami na wameunda makundi mengine na wanaipinga Dawat-e-Islami, bila ya misingi ya kisheria, wanajaribu kulidhoofisha kundi la Madanī linalolingania watu katika njia ya sawa. Kwa matlaba yao, silaha yao ni kusengenyua, uongo, kusemana vibaya, kushukiana vibaya, kutafutana makosa, kusambaza uvumi wa uongo na kukubali maneno ya uongo na wanadhani hii ni huduma kubwa mno kwa dini yetu. Basi wajizuie. Hii si huduma kwa dini bali ni matendo ya aibu ya daraja ya mwisho kabisa yanayojaza kitabu cha amali kwa madhambi.

Vile vile yeyote anayeshikamana na utambulisho wa Dawat-e-Islami, lakini bado anapinga Dawat-e-Islami, pia bila ruhusa ya kisheria na anakuza chuki katika nyoyo za waislamu, na anajaribu kuharibu hadhi na mbinu za Dawat-e-Islami; matendo hayo hayakubaliki katika sheria ya kiislamu.

Kusemana vibaya ni Ḥarām

Kwa kawaida mtu akimpinga mtu, basi hujaribu kwa vyovyote kutafuta makosa yake halafu hufanya bidii kutangaza na makosa yake (isipokuwa wale ambao wamelindwa na Allah ﷻ). Walipokuwa wanaelewana, ilikuwa kama vile jasho la mwenzake lanukia lakini sasa wametengana, basi hata uturi wake unakirihi.

Kumbuka! Kutangaza makosa na udhaifu wa mlinganizi hususan mwanachuoni wa kisunni, bila sababu ya kisawasawa ya kidini, kwa wengine husababisha hasara kubwa mno katika usambazaji wa dini na kazi ya kulingania watu katika haki. Na inaweza kusababisha adhabu ahera. ‘Alā-Ḥaḍrat Imām of Ahl-us-Sunnah, Maulānā, Ash-Shah Imām Aḥmad Razā Khān رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameleeza katika Fatāwā Razaviyyah: ‘Na kwa bahati mbaya iwapo mwanachuoni wa kisunni yeyote amefanya makosa, basi ni wajib kuficha, la sivyo watu hawatamuamini, Allah ﷻ asijaalie, na matokeo yake ni kwamba faida iliyokuwa ikipatikana katika hutuba na maandishi yake kuhudumia Uislamu na Sunna, zitaharibiwa. Allah ﷻ asijaalie, kutangaza na kuchapisha

makosa na udhaifu huu ni sawa na kueneza uchafu ambao umeharamishiwa ndani ya Quran Tukufu. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ
فِي الَّذِينَ آمَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ^ط

*Kwa hakika wale wanaopenda uenee uchafu kwa walioamini,
watapata adhabu chungu katika dunia na akhera.*

*[Kanz-ul-Īmān (Tafsiri ya Quran)] (Sūrah Nūr, Juz 18, Āyah 19)
(Fatāwā Raḍāwiyyah (Jad īd), juz. 29, uk. 594)*

صَلِّ اللّٰهُ تَعَالَى عَلٰى مُحَمَّدٍ صَلُّوا عَلٰى الْحَبِيبِ

Kutimiza masharti yote ya mapatano kwa wale waliotoka kutoka Dawat-e-Islami

Yeyote aliyetoka kutoka Dawat-e-Islami, ikiwa ameudhika na mimi au na Markazī Majlis-e-Shūrā, ikiwa nimewaudhi au nimeingilia haki zao kwa njia yoyote, nawaomba msamaha kwa unyenyekevu. Wanangu, Nigrān-e-Shūrā na wanakamati wa Markazī Majlis-e Shūrā wote wanataka msamaha wenu pia. Nawaomba munisamehe na muwasamehe kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ na Mtume wake Mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Kwa nia ya kumridhisha Allah عَزَّوَجَلَّ na Mtume wake صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ sote tumesamehe waliovunja haki zetu. Zaidi ya hayo, nawakaribisha

tena kurudi (Dawat-e-Islami) kwa mikono kunjufu wote wale ambao wameunda makundi yao na jumua zao, aidha kwa kukasirishwa na mtu fulani au kutoelewana na kundi. Nawaalika wote kwa moyo mkunjufu kupatana nami kwa ajili ya Allah ﷺ na Mtume wake ﷺ. Kwa nia ya kupata radhi za Allah ﷺ niko tayari kupatana bila masharti na kila ndugu muislamu ambaye amekasirika. Ndiyo, wale ambao wanataka kurekebisha mambo ya jumua kupitia mazungumzo, milango yetu iwazi kwa ajili yao. Tafadhali wasiliana na Markazi Majlis-e-Shūrā na ukae nao ukitaka pia mimi niwepo kwenye kikao nitahudhuria ikiwezekana. Njoo tuungane! Na kwa Rehema ya Allah ﷺ na jicho la huruma la Mtume wake ﷺ, ان شاء الله ﷺ, tuhudumie pamoja dini yetu na tuangamize mikakati miovu ya shetani.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ikiwa hutamani kufanya kazi na Dawat-e-Islami kisha...

Ikiwa ndugu yeyote muislamu aliyekasirika na hataki kujishughulisha na shughuli zozote za kimadani za Dawat-e-Islami basi angalau asitukasirikie na atusamehe; ili apate thawabu ya kumfurahisha muislamu mwenzake. Kwa njia hii chuki zitaondoka, mapenzi yatazidi na uso wa shetani utazidi kuwa mweusi na uso wa mwenye kusamehe utazidi kung'ara. Kwa mara nyingine tena nawaomba msamaha wenu kutokamana na maneno ya

Sultan wa Makka na Madina, kipenzi na Mtume Mteule wa Allah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, kama ilivyohadithiwa katika hadithi: ‘Aliyeombwa msamaha na ndugu yake muislamu na hakumsamehe (bila ya sababu ya kisheria) basi hatafikia chemichemi ya maji ya Kauthar¹.’

(Mu’jam Awsaṭ, juz. 4, uk. 376, Hadithi 6295)

Kumbuka si vizuri kusema kwamba [Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat, Muḥammad Ilyas ‘Aṭṭār Qādirī Razavī دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ] anakuja mwenyewe kwetu kuomba msamaha au amtumie Nigrān-e-Shūrā, au mwanakamati yeyote wa Markazī Majlis-e-Shūrā kwetu au kwa mkurugenzi wetu fulani. Mwenye kusema maneno haya anaweza kudhaniwa kuwa hataki maelewano na anatafuta sababu zisizokuwa za kimsingi.

Maadamu tushatangeliza ombi la msamaha kwa sura ya maandishi basi naona hakuna kizuizi tena kwa wenye ikhlas. Kila ndugu muislamu aliyekasirika asogee mbele kupatana. Ikiwa hataki kuja basi angalau awasiliane na mmoja kati ya wanakamati wa Markazī Majlis-e-Shūrā.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

¹ Chemichemi ya maji ya Kauthar au Ḥaḍ-e- Kauthar ni chemichemi ambayo Mtume wa Allah atatoa maji kwa wenye kiu Siku ya Kiyama. Kauthar ina maana ya neema.

Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Kuwa shahidi wangu

Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Kuwa shahidi wangu ya kwamba nimetangaza mwaliko wangu wa mapatano kwa ndugu zangu waislamu wasiridhika. Mola wangu **عَزَّوَجَلَّ**, watie huruma nyoyo zao ili waweze kunisamehe na tupatane. Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Wewe unaelewa hali ya nafsi yangu ninapoomba kupatana na wao; Lengo ni kuboresha ahera yangu.

Kabla ya kifo changu, nataka kuwaleta pamoja waislamu wote wasioridhika, nipatane nao kwa ajili yako; Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Nahofia hukumu yako; Mola wangu, Allah **عَزَّوَجَلَّ**, tafadhali usinikasirikie. Ewe Mtukufu Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Naomba katu imani yangu isiniondokee, hata kwa kipande kimoja cha sekunde. Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Nisamehe bila hesabu, pamoja na ndugu waislamu wasioridhika na wote walio na uhusiano na Dawat-e-Islami. Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ**! Usamehe umma wote wa kiislamu kwa ajili ya Kipenzi chako Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ**. Ewe Bwana wangu **عَزَّوَجَلَّ**! Tuletee umoja katika mistari yetu na utujaalie maelewano. Tafadhali tujaalie nguvu ya kuweza kuhudumia dini yako kwa pamoja, kwa ikhlasi bila ya tamaa ya kupata vyeo.

أَمِينٌ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Vita dhidi ya usengenyaji

Husikitisha sana! 'kusengenyaa kumewatia waislamu wengi utumwani'. Shetani awaburuta watu motoni kwa nguvu.

Tanabahini! Tangazeni vita dhidi ya usengenyaji na musibabaikie. Waliosengenywa, lazima watubie na wakazane kuomba msamaha. Amueni maamuzi makali kuwa: 'Hatutasengenywa wala kusikiliza masengenyoy!' **إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ**

Husikitisha sana! Usengenyaji umetafuna msingi wa mazingira ya Madanī kama mchwa. Kwa hivyo nawahimiza ndugu wote waislamu waliowajibika, wa kike na wa kiume, kwa lengo la kupigana vita dhidi ya usengenyaji watie kufuli milango yote ya usengenyaji. Waliojitenga na mazingira ya Madanī chini ya usimamizi wako, fikiria mara 112 kuhusu wao, pengine uliwatolea ukali kwa sababu walikusengenywa au wewe uliwasengenywa na ukawa sababu ya kuwavunja moyo na kuwakimbiza. Ikiwa hali hizi zote ni kweli, basi kwa nia safi na kwa ajili ya kupata radhi za Allah aliyetukuka **عَزَّوَجَلَّ**, waombe msamaha ikiwezekana huku machozi yakitiririka mashavuni mwako. Usiwaambie waje kwako lakini ombi langu la dharti ni wewe uwafuate na ujaribu kuwashawishi wakusamehe.

Na sio hawa tu, bali ndugu waislamu wote, waliotoka Dawat-e-Islami, napendekeza uwashawishi, uwaombe na uwanasihia na kwa vyovyote uwaregeshe katika mazingira ya haki ya Madanī ya Dawat-e-Islami na uwahusishe katika kutoa huduma ya kueneza Sunna. (Wale ambao hawana majukumu rasmi katika jumuiya, wanaweza kujihusisha katika upatanishi ila tu wasiwaguse wale ambao wametengwa rasmi na Dawat-e-Islami. Kesi zao zinashughulikiwa na wanakamati husika wa Dawat-e-Islami).

Nimemsamehe Ilyās Qādirī

Kwa ndugu wote waislamu wa kiume na wa kike, nawaomba kwa unyenyekevu ikiwa mimi, wanangu, Nigran au Arakin (wanakamati) wa Majlis-e-Shūrā tumemsengenya mmoja wenu au kumsingizia au kumkemea au kumuudhi au kumnyima haki yoyote kwa namna yoyote basi namuomba, tena namuomba, tena namuomba atusamehe na awe mwenye kupata malipo makubwa kwa Mwenyezimungu. Nasema tena kwa unyenyekevu asema angaa mara moja kwa roho safi, ‘Kwa ajili Allah عَزَّوَجَلَّ! Nimemsamehe Ilyās Qādirī Razavī, wanawe, Nigrane Shura na Arakine Shura.’ Na sisi sote vile vile kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ na Mtume wake صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, tumewasamehe wote waliotunyima haki ya aina yoyote kwa namna yoyote.

Ombi la Madani kwa wanaodai

Ikiwa wanidai au kama niliazima chochote kutoka kwao na sikuregesha, basi naomba uwasiliane na Nigrān-e-Shūrā wa Dawat-e-Islami au wanangu. Ikiwa hutaki kuregeshewa kitu chako, kwa ajili ya radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ, basi nisamehe na upate thawabu kubwa. Ninaowadai pesa zangu, nimewasamehe.

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيبِ

أَسْتَغْفِرُ اللهَ

تُوبُوا إِلَى اللهِ

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيبِ

Msichana bubu azungumza

Ndugu waislamu, ili kuondoa tabia ya kusengenya na kusikiza masengenyo na kukuza tabia ya kusali na kutekeleza sunna, jihusishe na mazingira maongofu ya Dawat-e-Islami. Hudhuria ijtimai ya kila wiki na usafiri na Madanī Qāfilāh pamoja na wafuasi wa Mtume ili kujifunza sunna. Ili kuneemeka katika maisha ya duniani na kufaulu kesho ahera tekeleza matendo yako kwa mujibu wa hojaji ya Madanī In'āmāt. Jaza kijitabu cha Madani In'amat na ukipeleke kwa msimamizi Madani In'amat katika siku kumi za kila mwezi wa Madanī [mwezi wa kiislamu]. Ili kukuvutia kuhudhuria ijtimai za kila wiki, hebu niwasilishe kisa cha ajabu cha Madanī.

Bila kutarajia, dada mmoja muislamu kutoka kijiji kilichoko wilaya ya Khūshāb (Pakistan) alipoteza sauti yake akawa bubu. Matibabu yote yakashindwa na akalepelekwa Bāb-ul-'Madīnah, Karachi (Pakistan). Matibabu huko pia hayakufaulu. Miezi sita ikapita akiwa katika hali hiyo hiyo. Halafu akabahatika kuhudhuria ijtimai ya kila wiki ya kina dada waislamu amabayo huanza saa nane na nusu alasiri kila Jumapili katika chumba cha chini kwa chini Dawat-e-Islami, Faizān-e-Madīnah. Kupitia juhudi za dada mmoja muislamu alihudhuria ijtimai kumi na mbili. Katika kuhudhuria ijtimai kwa mfululizo mara sita, Ramaḍhani ya 8 1430 A.H. Kufikia mwisho wa ijtimai hiyo, wakati wa kumsalia Mtume, **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ**, ghafla akazungumza.

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Baraka Za Sunnah

Katika maringira mazuri ya Dawat-e-Islami (Shirika la Kimataifa la Kaeneza Mafundisho ya Quran na Sunna liliojibusha na siana) sunna za Bwana Mtume ﷺ zinafanrusa kwa wingi.

Ni ombi kwa kila muislamu kuhudhuria na kukesha usiku mzima kwa nia ya kutaka radhi za Allah ﷻ pamoja na niya zingine nzuri katika jitima ya kila wiki siku ya Alhamisi baada ya sala ya Magharibi inayofanyika katika mji anacishi. Vile vile ni ombi kwa kila muislamu kusafiri na wapenzi wa Mtume ﷺ katika Madani Qafila kwa nia ya kupata thawabu na kujifunza sunna za Bwana Mtume ﷺ. Na afanye Fikr-e-Madina (kujisili mwenyewe) kwa kujaza kadi ya Madani In'amaat na amkabidhi Zimmedaar (msimamizi) wake katika siku kumi za mwanzo za kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivyo **بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ** tutaweka kushikamana na sunnah za Mtume ﷺ **حَسْبُكَ اللَّهُ يَا رَسُولَ اللَّهِ** na tutachukia maasi na tutatiki kuwa na harru ya kulinda imani yetu.

Kila muislamu aweke amna ya kwamba: "Nitajaribu kusubuhisha nafsi yangu na watu wote wa ulimwengu mzima" **بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ**

Kwa ajili ya kusubuhisha nafsi yangu nita fiuta Madani In'amaat na kusubuhisha nafsi za watu wa ulimwengu nita safiri katika Madani Qafila. **بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ**



www.dawateislami.net



MC 1266

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan.

UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 1262

Web: www.dawateislami.net | E-mail: translation@dawateislami.net